# HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KAWAIDA KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA MJI KIBAHA TAREHE 14 JANUARI, 2022.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mussa A. Ndomba | M/Kiti H/Mji Kibaha | Mwenyekiti |
| 2. | Eng. Mshamu A. Munde | Mkurugenzi H/Mji | Katibu |
| 3. | Mhe. Selina W. Msenga | M/Mkiti H/Mji Kibaha | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Goodluck N. Manyama | Diwani Kibaha | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hamis S. Shomari | Diwani Kongowe | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mfalme B. Kabuga | Diwani Tangini | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ramadhani A. Lutambi | Diwani Mailimoja | Mjumbe |

**MJUMBE ASIYEHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Silvestry F. Koka | Mbunge Kibaha Mjini | Mjumbe |
| 2. | Mhe Aziza A. Mruma | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |

**WATAALAM WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Sozi Ngate | Katibu Tawala Wilaya |
| 2. | George Mbogo | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 3. | Leah Lwanji | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 4. | Wambura Yamo | Mkuu wa Idara ya Mipango |
| 5. | Njau J. Marco | Mkuu wa Idara ya Kilimo |
| 6. | Optuna Kasanda | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 7. | Mkana M. Mkana | Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira |
| 8. | Jorum Mteka | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 9. | Peter Mallya | Mweka Hazina |
| 10. | Rosemary Msasi | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 11. | Benjamin Mputtu | Kaimu Afisa Tarafa Kibaha |
| 12. | Renitha Luzabiko | Afisa Tarafa Kongowe |
| 13. | Cecilia Mbagwire | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 14. | Adolph L. Msangi | Afisa Biashara |
| 15. | Cecilia Mushi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 16. | Aron Shushu | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango Miji. |
| 17. | Dr. Tulitweni Mwinuka | Mganga Mkuu |
| 18. | Bernard Ochieng | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |



Scanned with CamScanner

19. Mansuetha Mbena — Mkuu wa Kitengo cha Sheria
20. Bernadina Kahabuka — Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
21. Anitha Lyoka — Mratibu wa TASAF

**SEKRETARIETI**

1. Getruda Kalenzi
2. Gamcha Malongo

**KFU/MUHT. NA. 01/01/2022: KUFUNGUA KIKAO**

Baada ya akidi ya wajumbe kutimia, Katibu aliwasalimu wajumbe na kuwakaribisha katika kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha na Utawala kisha alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao.

Mwenyekiti aliwasalimu wajumbe na wataalam na kuwataka wajumbe kuwa makini katika kujadili taarifa kwa maslahi ya wananchi wa Halmashauri kisha alifungua kikao saa 05:00 asubuhi.

**KFU/MUHT. NA. 02/01/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA AJENDA**

Katibu alisoma ajenda mbele ya wajumbe Kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao.
2. Kusoma na kuthibitisha ajenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 15/12/2021 kawaida.
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 15/12/2021 kawaida.
5. Kujadili taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Disemba, 2021.
6. Kupitia mchakato wa kumpata dalali wa kufanya mnada wa jumla ya vibanda 197 vilivyomo katika soko la Mnarani Halmashauri ya Mji Kibaha.
7. Kujadili taarifa ya manunuzi kwa kipindi cha robo pili Oktoba hadi Disemba, 2021/2022.
8. Kupitia mchakato wa zabuni ya upelekaji maji Machinjio ya Mtakuja.
9. Kujadili taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Disemba, 2021
10. Mapokezi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa upimaji viwanja 20,000 mitaa ya Kidimu, Mkombozi na Lumumba kata ya Pangani.
11. Mapokezi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa zahanati ya Mwanalugali na ujenzi wa nyumba mbili za Watumishi wa afya zahanati ya Vikawe.
12. Taarifa ya utekelezaji wa hoja za ukaguzi wa ndani kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Disemba, 2021.
13. Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Idara/vitengo mbalimbali kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Disemba, 2021.
    - Idara ya Fedha na Biashara
    - Idara ya Utumishi na Utawala
    - Bodi ya zabuni na Kitengo cha manunuzi



Scanned with CamScanner

- Kitengo cha ukaguzi wa ndani
- Kitengo cha sheria
- Kitengo cha uchaguzi
- Kitengo cha mawasiliano, Habari, Uhusiano na TEHEMA

14. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
15. Kufunga kikao

Baada ya Katibu kusoma ajenda wajumbe walipokea na kuthibitisha ajenda 15 za kikao.

**KFU/MUHT. NA. 03/01/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 15/12/2021 KAWAIDA.**

Wajumbe walipitia muhtasari wa tarehe 15/12/2021 kawaida ukurasa kwa ukurasa na hakukuwa na masahihisho yoyote na waliridhia Mwenyekiti na Katibu kusaini muhtasari huo ili kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

**KFU/MUHT. NA. 04/01/2022: YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 15/12/2021 KAWAIDA.**

**Eneo la garden**

Kuhusu Kamati ya Fedha na Utawala kutembelea eneo la garden na kupitia upya mipaka ya eneo hilo na eneo la mbele ya Halmashauri, majibu yalitolewa kuwa eneo hili la garden ni eneo lililopo pembezoni mwa barabara ya Morogoro na barabara ya Halmashauri (bafer zone) eneo hili limetengwa kwa ajili ya kupanda miti ya kivuli na pia linaweza kutumika kwa ajili ya maegesho wakati wa shughuli za kitaifa.

Aidha ilielezwa kuwa Kamati hii itatembelea eneo hilo na kupitia mipaka tarehe 20.01.2022. Mjumbe mmoja alieleza kuwa Halmashauri ina eneo dogo na yule mpangaji pale analipa kodi Halmashauri hivyo kabla ya kwenda kutembelea eneo hilo ni vema watalaam wakajiridhishe kwanza. Mwenyekiti alieleza kuwa lengo la wajumbe ni kutaka kulitengeneza eneo hilo lipendeze na kuvutia kwani ni kioo cha Mji na lipo mbele ya Halmashauri.

Katibu alishauri kuwa baada ya kikao tutembelee eneo hilo, pia alieleza kuwa wazo ni zuri ila walifanya vikao na TANROADS na walielezwa kuwa wanaanza mradi wa ujenzi wa barabara njia sita hivyo suala hili litakuwa gumu kwani wameanza kufanya upembuzi yakinifu hivyo wakitembelea wajue kuna mradi huo.

Mwenyekiti alimtaka mjumbe aliye hudhuria kikao cha TANROADS kutoa ufafanuzi kwa faida ya kikao. Mtaalam huyoo alitoa maelezo kuwa barabara itakuwa ya njia sita kuanzia Mailimoja hadi TAMCO mita 121 kwa 121 na mita 45 kuanzia TAMCO hadi Chalinze. Kutokana na uwepo wa mradi huo Wajumbe walikubaliana kuwa suala hili lisubiri kwanza mpaka hapo mradi huo utakapoanza na kuona utekelezaji wake utaishia wapi.



Scanned with CamScanner

**Kuwasilisha stakabadhi za malipo**

Kuhusu kuandikwa kwa barua kwenda kwa NIC, PPRA, DDCA na Kigamure kuzitaka taasisi hizo kuwasilisha risiti ndani ya mwezi mmoja. Majibu yalitolewa kuwa agizo limetekelezwa barua ziliandikwa kwenda kwa taasisi za NIC, PPRA, DDCA na Kigamure na Taasisi hizo zimewasilisha risiti. Wajumbe walimtaka Mkaguzi wa ndani kuthibitisha kama amepokea risiti hizo, Mkaguzi wa ndani alithibitisha kupokea risiti hizo na kuwa hoja imefungwa hivyo wajumbe walikubaliana na utekelezaji uliofanyika.

**Mradi wa ujenzi wa nyumba ya mtumishi**

Kuhusu Mkuu wa Idara ya Ujenzi Eng. Brighton Kisheo na Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi Ndg. Alphonce Temba wapumzishwe kazi kupisha uchunguzi wa awali kutokana na mapungufu yaliyojitokeza katika ujenzi wa nyumba ya mtumishi (Ununuzi na matumizi yasiyoridhisha ya Mifuko ya simenti 492, Ununuzi na Matumizi yasiyoridhisha ya Nondo 208 na manunuzi ya Mchanga wenye thamani ya Sh. 5,950,000 manunuzi hayaendani na kazi iliyofanyika. Majibu yalitolewa kuwa agizo limetekelezwa wajumbe walikubaliana na utekelezaji uliofanyika.

**KFU/MUHT. NA. 05/02/2022: KUJADILI TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI OKTOBA HADI DISEMBA, 2021/2022.**

Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha robo ya pili kuanzia mwezi Julai hadi Disemba, 2021 iliwasilishwa kama ifuatavyo:-

**MAPATO.**

Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imekadiria kukusanya jumla ya **sh. 38,952,626,768.12** kutokana na mapato yatokanayo na ruzuku, mapato ya ndani na washirika wa maendeleo. Kwa robo ya pili ya kuanzia mwezi Oktoba hadi Disemba, 2021 **Shs. 13,497,789,233.06** zimekusanywa na kufanya jumla ya mapato kwa robo zote mbili kuanzia mwezi Julai hadi Disemba 2021 kuwa Shs **22,363,446,579.61** sawa na **57.4%** ya makisio ya mwaka 2021/2022.

**MAPATO YA NDANI.**

Halmashauri imekisia kukusanya jumla ya **Shs. 4,107,012,000.00** kutoka katika vyanzo vya ndani. Katika kipindi cha robo ya pili ya kuanzia mwezi Oktoba hadi Disemba 2021 zimekusanywa **Shs 1,136,322,659** na kufanya jumla ya mapato ya ndani kwa robo zote mbili kuwa ni **Shs 2,957,521,099.92** sawa na **72%** ya makisio ya mwaka 2021/2022. Kwa ujumla mapato ya ndani pamoja na vyanzo fungwa kwa mwaka 2021/2022 Halmashauri imekisia kukusanya **Tshs 4,561,367,650** na hadi kufikia robo ya pili inayoishia mwezi Disemba, 2021 Halmashauri imeweza kukusanya jumla ya **Tshs 3,151,896,148.39** na kufanya mapato ya ndani Kwa ujumla kufikia **69%** ya makisio ya mwaka 2021/2022.



Scanned with CamScanner

**MATUMIZI.**

Kwa mwaka 2021/2022 Halmashauri imekisia kutumia jumla ya **Tshs. 38,952,626,768.12** kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali Kwa wananchi wa Mji wa Kibaha. Katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali Kwa robo ya pili ya kuanzia mwezi Oktoba hadi Disemba mwaka 2021 zimetumika **Shs 12,016,913,300.74** na kufanya jumla ya matumizi kwa robo zote mbili kuwa **19,641,147,362.67** sawa na **50%** ya makisio ya mwaka 2021/2022.

**MATUMIZI YA BAKAA YA 2020/2021.**

Halmashauri illianza mwaka 2021/2022 tarehe 01 Julai, 2021 na bakaa ya **Shs. 1,694,815,022.21**. Kwa robo ya pili ya kuanzia mwezi Oktoba hadi Disemba 2021 zimetumika **Tshs. 219,118,556.05** na kufanya jumla ya matumizi ya bakaa kufikia **Tshs 996,414,744.23** sawa na **59%** na kubakiwa na kiasi cha **Tshs 698,400,277.98** ya makisio ya mwaka 2021/2022.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipokea na kuanza kuijadili kama ifuatavyo: Mwenyekiti alipongeza Menejimenti kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa asilimia 72 katika robo hii ya kwanza. Aidha, pamoja na vyanzo fungwa tumekusanya kwa asilimia 69 hivyo mwenyekiti aliwataka wakuu wa idara wanaohusika na vyanzo fungwa kuongeza bidii katika ukusanyaji wa mapato hayo.

**Stendi**

Mjumbe mmoja alitaka kujua kwanini mapato ya kituo yapo chini ya asilimia 50 ikizingatiwa kuwa kipindi cha Disemba, 2021 magari yalikuwa mengi. Maelezo yalitolewa kuwa Idara inaendelea kufanya maboresho na usimamizi hivyo wana imani kuwa kipindi cha Januari, 2022 mapato yataongezeka.

Mjumbe alieleza kuwa ni kweli kituo kinafanya kazi masaa 24 na magari yanaingia kituoni usiku lakini taa haziwaki kuna giza. Maelezo yalitolewa kuwa fundi amekwenda kuzikagua taa na ilionekana kuwa mfumo wa solar ni gharama kwa upande wa matengenezo hivyo Menejimenti imetafuta mafundi wa umeme ambao watafunga taa kwa gharama ya milioni tano hivyo suala hili lipo kwenye mchakato wa utekelezaji.

Mradi wa tofali.

Mjumbe mmoja alitaka kujua kuwa awali walielezwa kuwa zaidi ya shs 100,000,000 za fedha za UVIKO kwa ajili ya ujenzi wa madarasa zingetumika kununua tofali katika mradi wetu, lakini madarasa yamejengwa tayari na mpaka sasa hakuna mapato yaliyokusanywa katika kasma hiyo. Majibu yalitolewa kuwa wameuza tofali chache kutokana na bei kuwa kubwa wananchi hawakubaliani nayo. Aidha Katibu Tawala alienda Pangani na aliwataka kununua tofali Halmashauri kwani kinachotakiwa ni ubora hivyo wameanza kununua.

Aidha, mtaalam aliongezea kuwa kwa mujibu wa sheria ya Manunuzi itaonekana kuwa Mkurugenzi anawalazimisha kununua tofali katika mradi wa Halmashauri



Scanned with CamScanner

ambapo ni kinyume na utaratibu wa Manunuzi ambapo inahitajika ushindani hivyo aliomba kamati ya fedha kuongeza nguvu katika hili na ukizingatia ushindani ni mkubwa.

Mwenyekiti alieleza kuwa tutafute namna ya kuwabana ili wanunue tofali za Halmashauri na alishauri maelekezo yatolewe katika ngazi za chini kuwa wanatakiwa kununua tofali katika mradi wa Halmashauri na wataruhusiwa kununua nje, endapo Halmashauri tofali zitakuwa zimeisha kwani hiki ni chanzo cha mapato na aliitaka Menejimenti kuwasisitiza wasimamizi wa mradi katika kuimarisha ubora wa tofali kwa kuhakikisha zinakaa siku saba kabla ya kuuzwa ushauri ulipokelewa.

Mjumbe aliomba utolewe ufafanuzi kuhusu shs. 800,000,000 za ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya wakati kuna ujenzi unaendelea. Majibu yalitolewa fedha zilizotumika ni bakaa, fedha hizi ni za mwaka huu wa fedha na ili zitumwe Halmashauri zinatakiwa kuombwa Hazina na ajenda iliwasilishwa ajenda ya zabuni ya kutafuta fundi ujenzi na wajumbe wakaeleza kuwa ukamilishwe mchakato wa upatikanaji wa wazabuni wa kusambaza vifaa ambao uko hatua ya mwisho na utawasilishwa ili upatikane muhtasari wa kupeleka Hazina.

Baada ya majadiliano hayo wajumbe walipitisha taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha robo ya pili, Oktoba hadi Desemba, 2021.

**KFU/MUHT. NA. 05/02/2022: KUPITIA MCHAKATO WA KUMPATA DALALI WA KUFANYA MNADA WA JUMLA YA VIBANDA 197 VILIVYOMO KATIKA SOKO LA MNARANI HALMASHAURI YA MJI KIBAHA.**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha inatarajia kufanya mnada wa vibanda 197 vilivyopo katika soko la Mnarani ambavyo wafanyabiashara/wapangaji wamevitelekeza na asilimia kubwa hawajulikani walipo. Halmashauri imefanya jitihada zote za kuwatafuta wahusika kwa kutumika njia mbalimbali ikiwemo kutangaza katika eneo la soko kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kwa kutumia matangazo ya vipaza sauti, kubandika notisi ya siku 21 tarehe 13/7/2021 katika kila banda na maeneo mengine ndani ya soko na kutangaza/ kutoa notisi ya siku 14 katika gazeti la Habari leo la tarehe 22/10/2021.

**LENGO LA UPIGAJI MNADA**

Lengo kuu la kufanya mnada huo ilielezwa kuwa ni kupangisha fremu hizo kwa wafanyabiashara ambao wana nia ya kupanga na kuziendeleza fremu hizo na kulipa kodi Halmashauri na sio kwamba Halmashauri inauza na kukamilisha fremu hizo kwa wafanyabiashara.

**KUJADILI NA KUPITISHA DALALI WA MAHAKAMA.**

Halmashauri ya Mji wa Kibaha iliweza kuwasiliana na Mahakama na kumpata Dalali wa Mahakama (Coast Auction Mart Co.) wa kufanya kazi hiyo na kufanya mawasiliano nae kwa barua ya tarehe 24/11/2021 yenye Kumb. Na.



Scanned with CamScanner

KTC/J.10/3/VO.VI/10. Dalali huyo aliweza kujibu kwa barua ya tarehe 29/11/2021 na kueleza kukubali kufanya mnada huo na kutoa mchanganuo wa gharama za malipo ya utekelezaji wa kazi hiyo ya asilimia 10% kwa barua ya tarehe 13/12/2021.

Baada ya Ofisi ya Mkurugenzi kupata majibu hayo, iliteua timu ya majadiliano iliyohusisha wataalam kutoka idara ya fedha, Kitengo cha Biashara pamoja na sheria ili kuweza kufanya majadiliano na Dalali katika kipengele cha gharama za kazi husika. Dalali alikubali kupuguza gharama kutoka asilimia 10 hadi kufikia asilimia 7 ambapo gharama hizo za malipo zitalipwa kutokana na makusanyo ya madeni yatakayokusanywa na Halmashauri na sio gharama zitakazotokana na kunadishwa kwa fremu.

**MAAMUZI YA BODI YA ZABUNI**

Baada ya mchakato huo kukamilika, taarifa hiyo ya kusudio la kufanya mnada na taarifa ya Timu ya majadiliano iliwasilishwa katika kikao cha Bodi ya Zabuni ya Halmashauri cha tarehe 10/1/2021 na Bodi ya Zabuni iliridhia mnada ufanyike kwa kwa kumtumia Dalali huyo wa mahakama ambaye ni Coast Auction. Co. kwa gharama ambazo ziliafikiwa katika majadiliano. Wajumbe waliombwa kupitia taarifa hii na kuipitisha ili Halmashauri iweze kuendelea na taratibu za kimkataba ili kazi ifanyike.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe waliipokea na kuanza kuijadili kama ifuatavyo:- Mjumbe mmoja aliipongeza Menejimenti kwa hatua iliyofikiwa na alipongeza timu ya majadiliano kwa kuwezesha kupungua kwa gharama ya malipo ya Dalali kutoka 10% hadi 7%.

Mjumbe alitaka kujua idadi ya vibanda vitakavyopigwa mnada na majibu yalitolewa kuwa vibanda vipo 197 kati hivyo wamiliki wa vibanda 18 walifika ofisini na kufanya malipo hivyo mpaka sasa vibanda ambavyo vitapigwa mnada ni 174.

Katibu alikieleza kikao kuwa mnada unaendeshwa ili kulipa deni la kodi Halmashauri kwa mantiki hiyo kama mfanyabiashara atapata hasara ya fedha zake za ujenzi kutorudi Halmashauri itakuwa haihusiki kwani fedha itayokusanywa italipa deni fedha itakayobaki itarudishwa kwa wapangaji kwa ajili ya kufidia gharama za ujenzi.

Baada ya majadiliano hayo wajumbe waliridhia na kupitisha mchakato wa kumpata dalali wa kufanya mnada wa jumla ya vibanda 197 vilivyomo katika soko la Mnarani Halmashauri ya Mji Kibaha.



Scanned with CamScanner

**KFU/MUHT. NA. 06/02/2022: KUJADILI TAARIFA YA MANUNUZI KWA KIPINDI CHA ROBO PILI OKTOBA HADI DISEMBA, 2021/2022.**

Taarifa ya Manunuzi katika kutoa huduma mbalimbali Kwa wananchi wa Mji wa Kibaha iliwasilishwa ambapo ilionesha kuwa manunuzi haya yalifanyika Kama ifuatavyo kwa kila Idara.

| S/N | IDARA | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Idara Ya Utawala | 63,993,390.47 |
| 2 | Idara Ya Fedha | 54,237,196.50 |
| 3 | Idra Ya Afya | 38,551,037.66 |
| 4 | Idara Ya Elimu Msingi | 3,099,000.00 |
| 5 | Idara Ya Ujenzi | 664,800.00 |
| 6 | Mipangomiji | 71,432,300.00 |
| 7 | Kitengo Cha Nyuki | 100,000.00 |
| 8 | Kitengo Cha TEHAMA | 5,912,500.00 |
| 9 | Kitengo Cha Ukaguzi Wa Ndani | 3,296,100.00 |
| 10 | Mipango , Takwimu Na Ufuatiliaji | 30,352,500.00 |
| 11 | Idara Ya Kilimo | 2,802,450.00 |
| 12 | Idara Ya Elimu Sekondari | 12,758,598.80 |
| 13 | Idara Ya Maendeleo Ya Jamii | 3,599,100.00 |
| 14 | Kitengo Cha Biashara | 250,000.00 |
| 15 | Kitengo Cha Uchaguzi | 75,000.00 |
| 16 | Idara Ya Usafi Na Mazingira | 6,768,000.00 |
| | **JUMLA KUU** | **297,901,973.43** |

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuanza kuijadili kama ifuatavyo: Mjumbe mmoja alitaka kujua Halmashauri inahusika vipi na ununuzi wa vifaa vya kukarabati nyumba ya Mkuu wa Wilaya na maelezo yalitolewa kuwa Mkuu wa Wilaya ni sehemu pia ya Halmashauri kwani Halmashauri inahusika na ulinzi na usalama wa eneo lake hivyo ni jukumu pia la kuhakikisha Mwenyekiti wa ulinzi na usalama naye anaishi katika mazingira mazuri.

Kuhusu ununuzi wa vifaa vya usafi mjumbe alitaka kujua kwanini tunanunua vifaa wakati tuna kampuni. Majibu yalitolewa kuwa vifaa vinanunuliwa kwa ajili ya Stendi na kituo cha afya ambapo hakuna kampuni. Mwenyekiti alishauri kikao kijacho Menejimenti ishauri njia ipi ina gharama nafuu (ununuzi wa vifaa vya usafi pamoja na kulipa vibarua pamoja na kuingia mkataba na kampuni za usafi.

**AZIMIO:** Menejimenti ianishe gharama za kuingia mkataba na kampuni ya usafi na gharama za ununuzi wa vifaa na kulipa vibarua katika kituo cha mabasi.

Mwenyekiti alitaka kujua kuhusu mgawanyo wa mapato je idara zote zinatumia kadri wanavyoomba? Maelezo yalitolewa kuwa idara zote zinapata fedha kwa kuzingatia bajeti hata hivyo kuna vitengo, Katibu Tawala Mkoa wa Pwani ameagiza



Scanned with CamScanner

watengewe bajeti ya mapato ya ndani vitengo hivyo Ustawi wa jamii na Kitengo cha Afya Kinga (Maafisa Afya).

Baada ya majadiliano hayo wajumbe waliipitisha taarifa ya Manunuzi kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021.

**KFU/MUHT. NA. 07/02/2022: KUPITIA MCHAKATO WA ZABUNI YA UPELEKAJI MAJI MACHINJIO YA MTAKUJA.**

Taarifa iliwasilishwa ikiwa na utangulizi kuwa kitengo cha ugavi kilipokea dokezo kutoka kwa Mkurugenzi likiwa na maombi ya kumtafuta mtoa huduma atakaye peleka maji machinjio ya Mtakuja tarehe 13.12.2021 ambapo Tangazo la zabuni tajwa lilitolewa tarehe 14.12.2021 na ufunguzi ulitakiwa ufanyike tarehe 21.12.2021 lakini mpaka tarehe ya ufunguzi hakuna mzabuni/ mtoa huduma alieonesha nia ya kushirikiana na Halmashauri katika kutekeleza mradi huo.

Kitengo cha Manunuzi baada ya kupata ridhaa ya Bodi ya zabuni kiliweza kuwatafuta watoa huduma ambao walijishughulisha na huduma hiyo na kuweza kuwapatia nukuu zaa bei (quotation) na ufunguzi kufanyika tarehe 13.01.2022 na matokeo ya ufunguzi yalikuwa kama ifuatavyo;

1. Mgambakamo General Enterprises S.L.P 30365 Kibaha- Tsh 5,400,000 kwa mwezi.
2. Jaji Tayara investiment, S.L.P 30070 Kibaha –Tsh 4,500,000 kwa mwezi.
3. Oshiri& Family company Ltd, S.L.P 30882 Kibaha- Tshs 6,300,00

Aidha matumizi ya maji machinjio kwa siku ni lita 9,000 ambayo ni sawa na lita 270,000 kwa mwezi.

Kamati ya tathimini iliundwa na Mkurugenzi kwa kuhusisha wataalamu wafuatao:

1. Msafiri Thomas – Afisa Ugavi- Mwenyekiti
2. Latifa Maporo – Afisa Ugavi- Katibu
3. Zubeda Mwaruka- Afisa Mifugo – mjumbe.

**UCHAMBUZI WA KINA**

Kamati ya tathimini ilieleza kuwa uchambuzi wa kina *detailed evaluation* ulizingatia vigezo vilivyotolewa kwenye nyaraka ya zabuni.

**TATHIMINI YA MWISHO.**

Kwa kuwa wazabuni wote waliweza kukidhi vigezo vya awali vya msingi pamoja na kutokuwa na masahihisho ya kimahesabu kamati ya tathimini iliweza kuwapanga kuanzia mzabuni mwenye gharama ndogo kama ifuatavyo;

1. Mgambakamo General Enterprises- Tsh 5,400,00-02



Scanned with CamScanner

2. Jaji Taraya Investment- Tsh 4,500,000-01
3. Oshiri & Family Company Ltd-Tsh 6,300,000-03

**MAPENDEKEZO YA BODI YA ZABUNI.**

Bodi ya zabuni iliweza kuidhinisha kampuni ya JAJI TARAYA ya S.L.P 30070 Kibaha kupewa kazi hiyo kwa Tsh 4,500,000 kwa mwezi kwa ajili ya upelekeji wa maji lita 270,000 kwa mwezi ambayo ni sawa na lita 9,000 kwa siku katika machinjio ya Mtakuja .

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe waliipokea na kuanza kuijadili kama ifuatavyo:- Mjumbe mmoja alitaka kujua je kisima kilichochimbwa kinaweza kutoa maji. Majibu yalitolewa kuwa kisima kilichochibwa kinatoa maji ingawa ni maji ya chumvi. Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa Menejimenti iliona apatikane mzabuni wa kupelekeka maji kwa mkataba wa angalau miezi miwili wakati mawasiliano na DAWASA yanaendelea kwa ajili ya kupata gari la kusambaza maji machinjio kwa gharama nafuu.

Baada ya majadiliano hayo wajumbe waliipitisha mapendekezo ya Bodi ya Zabuni kuwa Kampuni ya JAJI TARAYA ya S.LP 30070 kupewa kazi kwa Tshs 4,500,000 kwa mwezi kwa ajili ya upelekaji wa maji lita 270,000 kwa mwezi ambayo ni sawa na lita 9000 kwa siku katika machinjio ya Mtakuja.

**KFU/MUHT. NA. 08/02/2022: KUJADILI TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI OKTOBA HADI DISEMBA, 2021/2022.**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye mpango na bajeti ya mwaka 2021/2022. Aidha, utekelezaji umefuata na kupitia malengo yaliyoanishwa katika Dira ya maendeleo ya Taifa 2025, malengo endelevu ya maendeleo (2016-2030) na maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na Wizara zinazosimamia sekta na ukomo wa bajeti iliyoelekezwa na Hazina kutumika kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapunduzi(CCM) ya mwaka 2020-2025 na sera mbalimbali za ki-sekta na kitaifa.

**MIRADI YA MAENDELEO**

Halmashauri ya Mji wa Kibaha imeendelea na majukumu ya kutoa huduma na kusimamia shughuli za miradi ya maendeleo kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilitolewa na serikali.

**Mpango wa mwaka 2021/2022 miradi ya maendeleo**

Kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Halmashauri ya Mji wa Kibaha imepanga kutumia jumla ya **Shs 14,510,285,835.00** ikiwa ni pamoja na fedha za bakaa ya mwaka 2020/2021 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shs. **1,814,804,800.00** ni za mapato ya ndani, Shs. **5,201,035,000.00** ni Ruzuku ya miradi kutoka serikali kuu na Mchango wa jamii na vyanzo vingine **ni Shs.**

**5,435,142,649.42** na fedha za bakaa ya mwaka 2020/2021 kutoka mapato ya ndani, serikali kuu na wafadhili wengine ni shs **1,387,239,024.58** kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

| Na. | CHANZO CHA FEDHA | FEDHA ILIYOIDHINISHWA 2021/2022 | FEDHA ILIYOTOLEWA HADI KUFIKIA DISEMBA, 2021. | ASILIMI A% |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato ya Ndani | 1,814,804,800.00 | 1,002,800,000 | 55.5 |
| 2. | Mchango wa Jamii | 100,000,000.00 | 52,342,800 | 52.3 |
| 3. | TASAF - PSSN | 574,435,000.00 | 302,743,324.28 | 52.7 |
| 4. | Ujenzi Jengo la Halmashauri | 1,000,000,000.00 | 174,732,853.69 | 17.5 |
| 5. | Elimu bure sekondari | 1,447,576,380.00 | 450,101,125.86 | 31.1 |
| 6. | Elimu msingi bila malipo | 634,125,620.00 | 192,268,478.98 | 30.3 |
| 7. | Ada za shule ya Msingi | 135,900,000.00 | 29,021,015.00 | 21 |
| 8. | Usafi wa mazingira-SWASH | 24,000,000.00 | 0 | 0 |
| 9. | Mfuko wa Pamoja (HSBF) | 251,346,000.00 | 49,305,868.26 | 19.6 |
| 10. | Mfuko wa Jimbo | 36,325,000.00 | 36,325,000.00 | 100 |
| 11. | Kuchangia NHIF | 101,909,250.00 | 45,198,150.00 | 44 |
| 12. | Kuchangia Papo kwa papo (USER FEE) | 142,546,400.00 | 79,522,026.30 | 56 |
| 13. | CHF/TIKA | 14,000,000.00 | 25,127,157.17 | 179 |
| 14. | Ruzuku ya afya-THPS | 21,000,000.00 | 0 | 0 |
| 15. | UNICEF | 10,000,000.00 | 0 | 0 |
| 16. | Gloal Fund | 35,062,000.00 | 0 | 0 |
| 17. | Vifaa tiba (MSD) | 238,119,724.00 | 0 | 0 |
| 18. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya | 800,000,000.00 | 0 | 0 |
| 19. | Mradi Mkakati (Soko la Kisasa) | 2,000,000,000.00 | 489,803,903.93 | 24.5 |
| 20. | Ruzuku ya Afya- RBF | 329,336,983.00 | 23,531,868.34 | 7.1 |
| 21. | NTD | 7,525,000.00 | 0 | 0 |
| 22. | Vaccine Delivery Report | 35,985,515.12 | 35,985,515.12 | 100 |
| 23. | Ujenzi wa shule mpya Sekondari | 1,075,200,000.00 | 470,000,000 | 43.7 |
| 24. | Elimu P4R Msingi | 346,581,500.00 | 0 | 0 |
| 25. | Elimu P4R Sekondari | 346,581,500.00 | 0 | 0 |
| 26. | Ujenzi wa MiundoMbinu Elimu Msingi | 112,000,000.00 | 112,000,000.00 | 100 |
| 27. | Ujenzi wa MiundoMbinu Elimu Sekondari | 112,000,000.00 | 0 | 0 |
| 28. | Ujenzi wa MiundoMbinu ya vyoo Elimu Sekondari | 64,510,000.00 | 0 | 0 |
| 29. | Ujenzi wa Madarasa Sekondari (Kodi ya miamala) | 37,500,000.00 | 37,500,000.00 | 100 |
| 30 | Drug Revolving Fund | 60,000,000.00 | 15,506,700 | 26 |
| 31 | Madarasa Sekondari (IMF) | 940,000,000 | 940,000,000 | 100 |
| 32 | Kituo cha Afya | 250,000,000 | 250,000,000 | 100 |
| 33 | COVID 19 (Ufuatiliaji na Tathimini) | 6,514,747 | 6,514,747 | 100 |
| 34 | COVID 19 Uhamisho wa chanjo | 10,137,391.3 | 10,137,391.3 | 100 |

| Na. | CHANZO CHA FEDHA | FEDHA ILIYOIDHINISHWA 2021/2022 | FEDHA ILIYOTOLEWA HADI KUFIKIA DISEMBA, 2021. | ASILIMI A% |
|---|---|---|---|---|
| 35 | Upimaji wa viwanja | | 1,588,000,000 | |
| 36 | Fedha za Bakaa ya mapato ya ndani ya mwaka 2020/2021 | 674,210,362.00 | 674,210,362.00 | 100 |
| 37 | Fedha za bakaa kutoka Serikali kuu na wafadhili wengine | 713,028,662.58 | 713,028,662.58 | 100 |
| | **JUMLA KUU MIRADI YA MAENDELEO** | **14,510,285,835.00** | **7,805,706,950** | **53.8** |

**TAARIFA YA UJENZI WA MADARASA 47 KWA FEDHA ZA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO 19**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha idadi ya shule zilizopata fedha ziko 13 na idadi ya madarasa ni arobaini na saba(47) fedha iliyopokelewa ni shs 940,000,000 na fedha iliyotumika ni 905,822,540.20 na bakaa ni shs 34,177,459.80 na jumla ya madawati 1,365 yamepatikana madarasa yote yalikuwa yamekamilika kujengwa.

**Matumizi**

Halmashauri ya Mji wa Kibaha imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kujumuisha fedha za Bakaa ya mwaka 2020/2021.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa iliwasilishwa wajumbe waliipokea na kujadili kama ifuatavyo:- Mjumbe mmoja alieleza kuwa fedha iliyoingizwa kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa Viti na meza katika shule ya Sekondari Mwambisi Forest ni shs. 5,000,000 lakini taarifa inaonesha kuwa shs. 10,000,000 ziliingizwa katika akaunti ya shule. Maelezo yalitolewa kuwa fedha hizo ziliingizwa shs 5,000,000 katika akaunti ya shule husika hivyo marekebisho ya taarifa yatafanyika.

**Ununuzi wa pikipiki**

Mwenyekiti alitaka ufafanuzi utolewe kuhusu ununuzi wa pikipiki kwa ajili ya watendaji wa kata na maelezo yalitolewa kuwa kibali kutoka ofisi ya Waziri Mkuu kimepatikana na tayari Menejimenti imeomba "specification" Wizara ya Ujenzi. Mjumbe mmoja alieleza kuwa taarifa inaonesha kuwa pikipiki zitanunuliwa kwa ajili ya watendaji wa kata wakati hoja ilikuwa ni ununuzi wa pikipiki kwa ajili ya maafisa ugani. Maelezo yalitolewa kuwa pikipiki zitanunuliwa na kugawiwa kwa kila kata na zitatumika na watendaji wa kata pamoja na maafisa wote waliochini yao.

Pamoja na maelezo hayo kutolewa mtaalam wa kilimo alieleza kuwa katika bajeti ametenga shs 5,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa pikipiki halikadhalika katika mwaka ujao ametenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa pikipiki hivyo itasaidia kupunguza changamoto ya usafiri kwa maafisa ugani. Pamoja na maelezo hayo ilitolewa taarifa kuwa tayari Halmashauri imepokea vibali vya pikipiki 14 za idara ya utawala



Scanned with CamScanner

pamoja na pikipiki mbili za idara ya kilimo na specification zimeombwa katika Wizara ya Ujenzi kama ilivyoelezwa hapo awali.

Mjumbe mwingine katika kuchangia hoja hii alishauri kuwa pikipiki zikabidhiwe kwa maelekezo maalum kuwa kuwepo ratiba maalum ya matumizi ya pikipiki hizo na kuwa si za mtu binafsi kwani Halmashauri haina uwezo wa kumnunulia kila mtendaji pikipiki. Katibu alikubaliana na hoja ya mjumbe kuwa pikipiki itakabidhiwa ofisi ya Mtendaji wa kata na kutumika na Watumishi wote wa kata na mitaa endapo watakuwa na shughuli.

**Machinjio ya kisasa Mtakuja**

Mjumbe alitaka kujua je machinjio ya kisasa Mtakuja inafanya kazi. Majibu yalitolewa kuwa mpaka sasa machinjio haifanyi kazi kutokana na kifaa kilichoharibika ambacho kilipelekwa kwa fundi na kimefanyiwa marekebisho na fundi wanaendelea na zoezi la kukifunga hivyo anategemea wiki ijayo machinjio itaanza kufanya kazi.

Mwenyekiti alitoa angalizo kwa Menejimenti kujiridhisha na muda wa matazamio wa mkandarasi wa vifaa ili Halmashauri isije ingia gharama ambayo inapaswa kulipwa na mkandarasi. Baada ya majadiliano hayo wajumbe waliipitisha taarifa ya miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021.

**Ujenzi wa madarasa 47**

Wajumbe walipongeza Menejimenti kwa kusimamia ujenzi wa madarasa 47 na kuyakamilisha kwa wakati na kuwezesha wanafunzi wote waliofaulu mitihani kujiunga na kidato cha kwanza. Aidha walimpongeza Mhe. Rais kwa kuona umuhimu wa kuipa kipaumbele sekta ya elimu sekondari.

Baada ya majadiliano hayo wajumbe walipitisha taarifa ya utekelezaji wa mradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Disemba, 2021.

**KFU/MUHT. NA. 09/02/2022: MAPOKEZI YA FEDHA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UPIMAJI VIWANJA 20,000 MITAA YA KIDIMU, MKOMBOZI NA LUMUMBA KATA YA PANGANI**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha imepokea fedha kiasi cha shilingi **1,588,000,000/=** kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikiwa ni mkopo usiokuwa na riba kutoka Serikali Kuu kwa lengo la kupanga na kupima viwanja **20,000** katika Mitaa mitatu ya Kidimu, Mkombozi na Lumumba. Aidha eneo hili linakadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta **2,963** sawa na ekari **7,407.5** lilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Mji Kibaha na Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, kwa ajili ya kupanga na kupima viwanja likiwa limelipiwa fidia lote lakini sehemu kubwa ilikuwa imevamiwa. Mpango huu wa utekelezaji unatokana na agizo alilolitoa Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenye



Scanned with CamScanner

mkutano wa hadhara uliofanyika na wananchi wa Kata ya Pangani tarehe **15/07/2021.**

***"Kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha aweze kupanga na kupima viwanja kwenye eneo la hekta 2963 ambalo limevamiwa na wananchi ili Halmashauri na serikali iweze kupata kodi na kuongeza mapato ya serikali kwa ujumla"***

**UTEKELEZAJI WA MRADI**

Katika kutekeleza mradi huu Halmashauri imepanga kutekeleza mradi huu kwa kufanya utambuzi kupanga na kupima viwanja kwa eneo lote ambalo Halmashauri ilikabidhiwa na Wizara ya Mifugo na uvuvi katika Mitaa ya Kidimu, Mkombozi na Lumumba ambapo zaidi ya viwanja **20,000** vinatarajia kupimwa. Hili kutekeleza mradi huu kwa muda mfupi kwa ufanisi na Amani, Kamati tano zitaundwa ambazo zitashirikisha uongozi wa Mkoa, Wilaya, na Halmashauri.

**KAMATI**

Ili kufanikisha mradi na kuhakikisha mradi unakuwa wa ufanisi na unatoa mafanikio mazuri.

Kamati zifuatazo zitaundwa.

i. Kamati ya Uongozi
ii. Kamati ya Uhamasishaji
iii. Kamati ya wataalam (Technical committee)
iv. Task Force
v. Vikao vya kisheria.

**KAMATI YA UONGOZI**

Kutakuwa na kamati ya uongozi ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao

1) Mkuu wa Mkoa-Mwenyekiti
2) Katibu Tawala wa Mkoa
3) Mkuu wa Wilaya
4) Katibu Tawala wa Wilaya
5) Mkurugenzi wa Halmashauri
6) Mwenyekiti wa Halmashauri
7) Mwenyekiti wa kamati ya Mipangomiji
8) Mwenyekiti wa CCM- Mkoa
9) Mwenyekiti wa CCM –Wilaya
10) Kamishna wa Ardhi
11) DSO
12) RPC
13) RSO
14) OCD



Scanned with CamScanner

**UHAMASISHAJI.**

Kutakuwa na Kamati ya uhamasishaji ambayo lengo lake litakuwa na kutoa uelewa na hamasa kwa wananchi na kuhakikisha mradi unaeleweka na kufanyika kwa Amani ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao.

1) Mkuu wa Mkoa
2) Mkuu wa wilaya
3) Katibu Tawala Wilaya
4) Mwenyekiti wa Halmashauri
5) Mkurugenzi wa Halmashauri
6) Mwenyekiti wa CCM -Wilaya
7) Mbunge
8) Madiwani
9) Afisa maendeleo ya jamii
10) Afisa Tarafa
11) Mwanasheria na
12) Afisa habari

**KAMATI YA WATAALAM (TECHNICAL COMMETTEE)**

Kutakuwa na kamati ya wataalam ambayo itafanya vikao vitatu kila mwezi na itakuwa na wajumbe wafuatao:-

1) Mkurugenzi wa Halmashuri ya Mji - Mwenyekiti
2) Kamati ya uongozi(CMT)
3) Katibu Tawala Wilaya
4) Kamishna wa Ardhi
5) Afisa Tarafa
6) Meneja TARURA
7) Mwakilishi TANESCO
8) Mwakilishi DAWASCO

**TASK FORCE**

Kutakuwa na kamati ya wataalam ambayo itakuwa na jukumu la kufuatilia utekelezaji wa mradi kila siku na itatakiwa kukutana kwa kila wiki mara moja na kuandaa taarifa ya kitaalam ya utekelezaji wa Mradi ya kila wiki ambayo itawasilishwa kwa Kamishna wa Ardhi.

1) Afisa Mipangomiji wa Mkoa
2) Mpima Ardhi wa Mkoa
3) Mthamini wa Mkoa
4) Mkuu wa Idara Mji Kibaha
5) Wakuu wa Vitengo vya Ardhi
6) Mwanasheria
7) Mwakilishi wa Kamishna Msaidizi

**VIKAO VYA KISHERIA**



Scanned with CamScanner

Kutakuwa na Kamati inayohusisha wajumbe wa vikao vya kisheria vya Halmashauri ya Mji Kibaha ambao ni watatakiwa kupewa taarifa na kutathmini maendeleo ya mradi.

1) Wajumbe wa Kamati ya Mipangomiji na Mazingira.
2) Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala.
3) Baraza la Madiwani.

## 1. KAZI ZIFUATAZO ZITAFANYIKA

i. Utambuzi wa mipaka ya wananchi waliomo kwenye eneo hilo na kuandaa ramani za msingi (basemap) na michoro ya mipangomiji
ii. Kupima viwanja.
iii. Umilikishwaji.

## I. UTAMBUZI NA UANDAAJI WA MICHORO YA MIPANGOMIJI

Kazi ya utambuzi na utayarishaji wa michoro ya mipangomiji itaenda sambamba na itahusisha watalaam wa sekta zote za ardhi pamoja na mahitaji yao kama ilivyoorodheshwa chini

i. Maafisa Mipangomiji
ii. Wapima Ardhi
iii. Maafisa ardhi
iv. Wathamini
v. Dereva
vi. Mrasimu Ramani
vii. Material for drawing (plotters, catridges)

## II. UPIMAJI

Katika hatua hii ya upimaji jumla ya makundi tisa yenye wataalam walioorodheshwa chini na mahitaji yatashiriki na kila kundi litatakiwa kupima jumla ya viwanja (2500) elfu mbili na miatano.

i. Wapima Ardhi
ii. Wapima Wasaidizi
iii. Vibarua (casual labour)
iv. Viongozi wa Mtaa
v. Madereva
vi. Vifaa vya upimaji
vii. Beacons

## III. UMILIKISHWAJI

i. Afisa Ardhi
ii. Afisa Ardhi Msaidizi
iii. Record Officers
iv. Vifaa vya umilikishaji



18. Mansue



Scanned with CamScanner

- Files
- Crested papers

IV. **MANUNUZI YA VIFAA**

- Nondo
- Cement
- Transportation of beacon
- Panga
- Sped / sululu
- Drafting films
- Stationaries (A1, A0, A3 & A4.)
- Manunuzi ya Printer(Heavy Duty printer)
- Manunuzi ya Photocopy machine
- Printers(3)
- Wino wa Plotter cartilages and Printers
- Manunuzi ya vifaa 3 vya kisasa cha upimaji (RTK with 2 rovers)
- Computers(3)
- Deasel
- Matengenezo ya gari
- Rake (3) za kuhifadhia majalada masijala
- Vifaa vya uchoraji (Rotrin)
- Maker pen, file tags (green tags)
- Pen (blue, black & red) box 5 kila moja
- Furniture (viti, meza na kabati)

**2. BAJETI YA MRADI**

Mradi huu utatekelezwa kwa jumla ya **Tshs 1,588,000,000** ambazo zimetolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Mkazi kama mkopo usiokuwa na riba.

**HALI HALISI YAUTEKELEZAJI**

Katika kutekeleza mradi huu wa kupanga na kupima viwanja 20,000, Halmashauri imejipanga kufanya kazi zifuatazo:-

i. Utambuzi wa wananchi waliovamia eneo hilo.
ii. Kuandaa michoro ya mipangomiji.
iii. Kupima viwanja.
iv. Kumilikisha viwanja kwa mujibu wa utaratibu utakaowekwa na Halmashauri kutokana na maagizo ya Waziri.

Mpaka sasa Halmashauri imekamilisha zoezi la utambuzi wa wananchi waliovamia eneo hilo katika Mtaa wa Kidimu. Hatua inayoendelea sasa ni ya kupima viwanja na kutoa elimu ya umilikishwaji.



Scanned with CamScanner

Kazi hii ni kubwa Halmashauri imepanga kutekeleza kwa muda wa miezi minne (4) hadi mwezi Aprili kazi ya kupanga na kupima Mitaa yote ya Kidimu, Mkombozi na Lumumba itakuwa imekamilika.

Aidha kutokana na mradi huu mkubwa Halmashauri na Serikali kwa ujumla wanategemea kupata mapato makubwa yatakayotokana na mradi huu. Waheshimiwa Madiwani waliombwa kushirikiana na wataalam katika zoezi la uhamasishaji kwa jamii yote.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe walipokea na kuanza kuijadili kama ifuatavyo; Mjumbe mmoja alishauri kuwa ni vema kikafanyika kikao cha ndani cha viongozi kabla ya kwenda kufanya kikao na wananchi lengo ni wajumbe wote wawe na uelewa wa pamoja.

Mjumbe mwigine aliongezea kuwa awali tulikuwa na mradi huu lakini hatukuwa wamoja hivyo aliunga mkono hoja ya kuwa na kikao cha ndani kabla ya kwenda kwa wananchi. Aidha alimshauri Mwenyekiti kuwa atakayeenda kinyume na matakwa ya mradi huu atachukuliwa hatua mara moja alisisitiza kuzingatia yale yaliyopangwa vizuri na wataalam.

Mjumbe mwingine alieleza kuwa Diwani wa kata ya Pangani amekuwa akikwamisha utekelezaji wa mradi huu aliunga hoja kuwa hatua stahiki zichukuliwe kwa wote watakaokwamisha mradi huu.

Mwenyekiti alikieleza kikao kuwa suala hili halina siasa kwani Halmashauri inategemea kupata mapato kutokana na mauzo ya viwanja hivyo alipongeza Idara kwa kuiwezesha Halmashauri kupata mradi huu ambao utaongeza mapato ya Halmashauri na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Katibu aliekieleza kikao kuwa Watendaji wamepokea maelekezo ya wajumbe na kuwa wanatambua athari zitakazojitokeza endapo Halmashauri itashindwa kutekeleza mradi huu kwani fedha iliyotolewa ni ya mkopo kwa dhana kwamba ardhi ipo na Wizara ina Imani kuwa mradi huu utatekelezeka hivyo suala hili lilipokelewa na wataalam kwa msisitizo mkubwa.

Baada ya majadiliano hayo wajumbe walikubaliana na taarifa ya Mapokezi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa upimaji viwanja 20,000 mitaa ya Kidimu, Mkombozi na Lumumba kata ya Pangani.

**KFU/MUHT. NA. 10/02/2022: MAPOKEZI YA FEDHA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UJENZI WA ZAHANATI YA MWANALUGALI NA UJENZI WA NYUMBA MBILI ZA WATUMISHI WA AFYA ZAHANATI YA VIKAWE.**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa Halmashauri ya mji wa Kibaha ni miongoni mwa Halmashauri tisa za Mkoa wa Pwani zinazotekeleza mradi wa TASAF chini ya Mpango wa kunusuru kaya masikini. Mpango huu kwa kuwalipa walengwa ruzuku



Scanned with CamScanner

ya miezi miwili. Pamoja na uhawilishaji wa fedha, TASAF inajihusisha na miradi mahsusi (Targeted infrastuctures- TI) ambayo hujenga miundombinu kwa ajili ya kuboresha huduma za jamii kwa eneo husika.

Kupitia mradi huu, Halmashauri ya Mji imepata fedha 2021/2022 kutoka TASAF makao makuu kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa Zahanati ya Mwanalugali na ujenzi wa Nyumba ya Watumishi (2 in 1) Zahanati ya Vikawe. Tarehe 29 Disemba, 2021 Mkurugenzi wa mji alipokea barua ya kuingiziwa fedha Tshs **204, 160, 714.28** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo, ambapo kila mradi umepata Tshs. **102, 050, 357.14.**

**TATIZO**

Vifo hasa vya akina mama wajawazito na watoto vinavyotokana na ukosefu wa zahanati ukosefu wa Watumishi wa afya hasa nyakati za usiku.

**LENGO**

Lengo la miradi ni kuboresha afya za wakazi wa Mitaa husika na mitaa ya jirani.

**UIBUAJI WA MIRADI**

Kupitia program hii, miradi miwili iliibuliwa ambayo;

1. Ujenzi wa Zahanati ya Mwanalugali.
2. Ujenzi wa Nyumba ya Watumishi zahanati ya Vikawe (2 in 1).

**UTHIBITISHO WA MRADI.**

Timu kutoka Halmashauri ya Mji kibaha ilitembelea mtaa wa Mwanalugali-A na Vikawe shule kwa ajili ya uthibitisho wa miradi kupitia mikutano maalumu ya wananchi. zaidi ya 50% ya wakazi wenye uwezo wa kupiga kura wa mitaa yote miwili walithibitisha na kuikubali miradi.

**GHARAMA ZA MIRADI**

Kila mradi utagharimu kiasi cha Tshs 102,080,357.14. Ofisi ya TASAF imetoa gharama za vifaa na fundi, jamii itachangia 10% ya mradi ambayo ni kuchota maji, kusaidia fundi, kusafisha eneo, ulinzi, utunzaji wa vifaa.

**MUDA WA MRADI**

Miradi unategemewa kuchukua muda wa mwaka mmoja mara utakapoanza.

**MATOKEO YA MRADI**

Baada ya kumalikiza kwa miradi hii, afya za wakazi wa mitaa ya Mwanalugali-A na Vikawe shule zitaboreka pamoja na kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga kinachochangiwa na ukosefu wa huduma ya zahanati na upatikanaji wa Watumishi wa afya hasa nyakati za usiku.

**SHUGHULI ILIYOFANYIKA MPAKA SASA.**

Shughuli iliyofanyika mpaka sasa katika miradi hii ni uchaguzi wa kamati ya usimamizi wa miradi (CMC) kwa kila mtaa, ambayo itakuwa na jukumu la



Scanned with CamScanner

kusimamia mradi kwa kuwa miradi hii inasimamiwa na jamii husika. Utekelezaji wa miradi hii utaanza mwezi Januari, 2022

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe waliipokea na kuipitisha taarifa ya mapokezi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa zahanati ya Mwanalugali na ujenzi wa nyumba mbili za Watumishi wa afya zahanati ya Vikawe.

**KFU/MUHT. NA. 11/02/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA HOJA ZA UKAGUZI WA NDANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI OKTOBA HADI DISEMBA, 2021/2022.**

Taarifa iliwasilishwa ikiwa na Utangulizi, Madhumuni ya ukaguzi, Mawanda ya ukaguzi, Utekelezaji wa hoja Kwa kipindi kilichopita, yaliyojitokeza Kwenye Ukaguzi Kwa kipindi cha robo ya pili, Oktoba hadi Desemba, 2021 Ukaguzi wa mapato, Ukaguzi wa matumizi, Malipo yenye viambatanisho pungufu, Masurufu ambayo hayajarejeshwa. Malipo yaliyofanyika bila kufuata taratibu za ununuzi. Ukaguzi wa Malipo ya miradi ya maendeleo.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe waliipokea.

**KFU/MUHT. NA. 12/02/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA IDARA/VITENGO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI OKTOBA HADI DISEMBA, 2021/2022.**

**IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa katika kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021 Idara ya Utumishi na Utawala imejikita katika kutekeleza shughuli zifuatazo;-

1. **Kusimamia na kuratibu uendeshaji wa vikao vya Halmashauri**

Idara imeratibu na kusimamia vikao vyote vya Halmashauri. Aidha Idara imehamasisha ufanyikaji wa vikao vyote vya kisheria katika ngazi za idara, Kata (WDC) na Mitaa katika Halmashauri ya Mji Kibaha ili kutekeleza na kusimamia dhana nzima ya Utawala Bora.

Vikao vilivyofanyika ni kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| • Baraza la Madiwani | 2 |
| • Kamati ya Fedha na Utawala | 4 |
| • Kamati ya Huduma za uchumi | 1 |
| • Kamati ya Mipango Miji na Mazingira | 1 |
| • Vikao vya CMT | 7 |
| • Kamati ya Kudhibiti UKIMWI | 1 |
| • Kamati ya Maadili | 1 |
| **JUMLA** | **17** |

2. **Masuala mbalimbali ya kiutumishi**



Scanned with CamScanner

Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021 Idara imeweza kufuatilia masuala mbalimbali yanayohusu haki za watumishi, ikiwa ni pamoja na kuwathibitisha kazini watumishi, kuwabadilisha vyeo watumishi 121, madeni, mafao na pensheni za watumishi wastaafu, kufuatilia masuala ya Kinidhamu pamoja na mazoezi ya kitaifa ya uhakiki wa vyeti vya watumishi na kusafisha taarifa za watumishi katika Mfumo. Aidha Idara ya Utumishi na Utawala inaendelea na shughuli ya maandalizi ya bajeti ya mishahara ya watumishi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika mfumo mpya wa kiutumishi New HCMS pamoja na mfumo wa PLAN REP.

3. **Kuwezesha shughuli za usafi na ulinzi wa maeneo ya ofisi za Mji.**
Idara imeweza kusimamia na kuratibu shughuli zote za ulinzi na usafi wa mazingira katika maeneo yanayozunguka Ofisi ya Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji Kibaha.

4. Taarifa za watumishi Ajira mpya mmoja (1), Waliohama tisa (9), waliohamia ishirini na tano (25), walioacha kazi hakuna, waliofariki mmoja (1), Waliostaafu watatu (3).

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe waliipokea na kuipitisha taarifa ya Idara ya utumishi na utawala kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021.

**IDARA YA FEDHA NA BIASHARA**
Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa Idara ya Fedha na Biashara kwa kipindi cha robo ya pili, 2021 imeweza kutekeleza shughuli/majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/2022.

**SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA**

**A. KURATIBU SHUGHULI ZA UKUSANYAJI MAPATO**
Halmashauri kwa robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa pamoja wameweza kufanikisha ukusanyaji mapato ya ndani kwa jumla ya Tshs. **1,136,322,659** na kufanya jumla ya mapato ya ndani kwa robo zote mbili kuwa 2,957,521,099.92 sawa na asilimia **72** ya makisio ya mwaka 2021/2022 ambayo ni **Tsh. 4,107,012,000.**

Aidha hadi kufikia robo pili Halmashauri imekusanya mapato toka kwenye vyanzo fungwa jumla ya **Tshs. 3,151,896,148.39 na** kufanya jumla ya mapato yote ikijumuisha mapato ya ndani na vyanzo fungwa kufikia 69% ya makisio ya mwaka 2021/2022.

Kufanya zoezi la ufuatiliaji, ukaguzi, na kutoa elimu kwa walipa kodi na ushuru wa Halmashauri kila wiki kwa kushirikiana na wakuu wa Idara na vitengo pamoja na timu za ufuatiliaji mapato.



Scanned with CamScanner

**B. KURATIBU SHUGHULI ZA MATUMIZI YA HALMASHAURI**

i. Kwa kushirikiana na idara nyingine kuandaa makisio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.
ii. Kuandaa malipo mbalimbali kwa Idara na Vitengo vyote vya Halmashauri ya Mji kwa kutumia mfumo wa MUCE
iii. Kushirikiana na timu za ukusanyaji wa mapato katika kazi ya ukusanyaji wa mapato
iv. Kuandaa majibu ya Mkaguzi wa ndani kwa kipindi cha robo ya kwanza.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe waliipokea na kuipitisha taarifa ya Idara ya Fedha na Biashara kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021.

**KITENGO CHA MANUNUZI NA BODI YA ZABUNI**

**KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA KITENGO CHA UNUNUZI**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa katika robo ya pili ya mwaka 2021/2022 kitengo cha Ununuzi kimetekeleza kazi zifuatazo ambazo ziko katika Mpango wa Ununuzi na Bajeti.

- Hati za kuagiza vifaa mbalimbali zimeandaliwa kupitia mfumo mpya wa MUSE na vifaa hivyo kupokelewa na kusambazwa kwa watumiaji/waagizaji na kuingizwa katika vitabu vya stoo(ledger book)
- Manunuzi yote yaliweza kufanyika kwa mfumo wa TANePS.

**KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA BODI YA ZABUNI.**

Bodi ya zabuni kwa kipindi cha miezi mitatu ya kuanzia Oktoba- Desemba, 2021 imeweza kuidhinisha Manunuzi yote yaliyofanyika kipindi cha robo ya pili.

**CHANGAMOTO**

1. Uelewa Mdogo wa sheria Mpya ya Ununuzi ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013 katika kuisoma na kuitafsiri kwa Idara Tumizi na watumishi wengine wanaotoka Idara zinazoshughulikia ununuzi kama vile walimu wakuu,watendaji wa mitaa na kata pamoja na kamati za ujenzi.

**UTATUZI WA CHANGAMOTO**

- Kutoa elimu kwa ngazi za chini kuhusiana na njia bora ya ununuzi.
- Kuwahimiza wazabuni wa Kibaha kujisajili katika mfumo wa ununuzi wa TANePS).

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe waliipokea na kuipitisha taarifa ya Kitengo cha Manunuzi na Bodi ya zabuni kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021.

**KITENGO CHA SHERIA**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa Kitengo cha Sheria husimamia utekelezaji wa Sheria na Taratibu zinazoratibu shughuli mbalimbali za Halmashauri kupitia idara

zake zote na majukumu yake ni mtambuka. Katika kipindi cha robo ya pili Kitengo cha Sheria kimetekeleza kazi zifuatazo:

**SHUGHULI AMBAZO ZIMETEKELEZWA**

Katika kipindi cha robo ya pili, Kitengo cha Sheria kimetekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kuiwakilisha Halmashauri katika mashauri mbalimbali yaliyoko Mahakamani ambapo kwa sasa Halmashauri ina jumla ya kesi 12 bado zinaendelea Mahakama Kuu Dar es Salaam na kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba Kibaha (***angalia kiambatisho***).

(ii) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Mkurugenzi, Wakuu wa Idara, pamoja na wadau mbalimbali wa Halmashauri kila mara inapohitajika kufanya hivyo.

(iii) Kitengo cha Sheria kimeweza kuandaa majibu ya hoja za kesi mbalimbali ambazo zinaendelea dhidi ya Halmashauri katika Baraza la Ardhi na Nyumba Kibaha.

(iv) Kitengo kimepitia na kuandaa mikataba mbalimbali ya Halmashauri ili kuhakikisha maslahi yanalindwa kabla ya kusaini na wateja wake.

(v) Kitengo kimeweza kutoa ushauri, elimu na msaada wa kisheria kwa jamii hususani wananchi wasio na uwezo.

(vi) Kitengo kimeshiriki katika mikutano na vikao mbalimbali vya Halmashauri.

(vii) Kitengo kimeshiriki kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo.

**MAFANIKIO**

(i) Kumaliza kesi kwa ufanisi na kuwezesha Halmashauri kushinda katika kesi nyingi.

(ii) Kutoa, ushauri, elimu na msaada wa kisheria kwa jamii inayotuzunguka ambao wana uhitaji na huduma ya kisheria na hawana uwezo wa kuipata na kushiriki katika utatuzi wa migogoro mbalimbali hususani migogoro ya ardhi.

(iii) Kuandaa mikataba yenye tija kwa maslahi ya Halmashauri.

(iv) Kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo kwa ufanisi hivyo kuwezesha kupunguza kesi zisizo za lazima kwa Halmashauri.

***KIAMBATISHO***

| S/N | NAMBA YA SHAURI NA JINA LA MAHAKAMA | WADAAWA | KIINI CHA KESI | MADAI/THAMANI YA SHAURI | HATUA ILIYOFIKIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 101/2016<br><br>MAHAKAMA KUU DIVISHENI YA ARDHI DAR ES SALAAM | Gideon John Mwikola na wenzake 19 dhidi ya KTC na St. John Bosco Parish | Mgogoro wa madai ya fidia eneo la Air Msae Kibaha lililochukuliwa na St. John Bosco Parish. | Madai ya fidia kiasi cha shilingi 990,000,000/= | Ipo katika hatua ya kusikilizaMahakama Kuu Dar es Salaam na imepangwa tarehe 25/1/2022 |



Scanned with CamScanner

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | 102/2017<br><br>BARAZA LA WILAYA LA ARDHI NA NYUMBA KIBAHA | Simon Rhodes Gau dhidi ya KTC na wenzake 31 | Mgogoro wa uvamizi wa ardhi ekari 100 eneo la Vikawe | 40,000,000/= | Ipo katika hatua ya kusikiliza Baraza la Ardhi na Nyumba Kibaha na imepangwa tarehe 9/3/2022. |
| 3. | 178/2016<br><br>BARAZA LA WILAYA LA NYUMBA NA ARDHI KIBAHA | Mwanaidi Abdallah Juma dhidi ya KTC na wengine | Mgogoro wa uvamizi wa ardhi eka 25 eneo la Vikawe | 45,000,000/= | Ipo katika hatua ya kusikiliza Baraza la Ardhi na Nyumba Kibaha na imepangwa tarehe 2/3/2022. |
| 4. | 652/2019<br><br>MAHAKAMA KUU DIVISHENI YA ARDHI DAR ES SALAAM | Laban R. Mapangwa dhidi ya KTC wengine 3 | Maombi madogo ya kuomba kurudisha rufaa iliyotupiliwa mbali kwa kutohudhuria Mahakamani | 18,000,000/= | Maombi hayo yalikubaliwa na sasa ipo katika hatua ya kusikiliza rufaa iliyoombwa na mdai Mahakama Kuu Dar es Salaam. |
| 5. | 79/2018<br><br>BARAZA LA WILAYA LA ARDHI NA NYUMBA KIBAHA | Juma Nassoro dhidi ya KTC | Mgogoro wa uvamizi wa ardhi eneo la ekari sita eneo la Kidimu | 65,000,000/= | Ipo katika hatua ya kusikilizwa Baraza la Ardhi na Nyumba Kibaha na imepangwa tarehe 10/2/2022. |
| 6. | 84/2019<br><br>BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIBAHA | Tuponile Nyaki dhidi ya KTC | Madai ya fidia shilingi 250,000,000/= ya eneo lililopo Lulanzi Picha ya Ndege (CBD AREA) | 250,000,000/= | Ipo katika hatua ya kusikilizwa kwa upande wa wadai Baraza la Ardhi na Nyumba Kibaha na imepangwa tarehe 22/3/2022. |
| 7. | 174/2019<br><br>BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIBAHA | James Geofrey Na Mwenzake Nyaki Dhidi ya KTC | Madai ya fidia shilingi 250,000,000/= ya eneo lililopo Lulanzi Picha ya | 250,000,000/= | ipo katika hatua ya kusikilizwa kwa upande wa utetezi Baraza la Ardhi na Nyumba Kibaha na |



Scanned with CamScanner

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ndege (CBD AREA) | | Imepangwa tarehe 22/3/2022. |
| 8. | 181/2020 MAHAKAMA KUU KITENGO CHA ARDHI | Paulo Brake Kaswalala na wenzake dhidi ya Benny Shelukindo Nchanjala, KTC, Sg, Registrar of Tittle na wenzake | Mgogoro wa ardhi Plot No. 262-317 kuwa Shelukindo amemilikishwa bila kufuata utaratibu | 100,000,000/= | Shauri lipo katika hatua za awali za kutajwa na kuandaa na kuwasilisha nyaraka mbalimbali na imepangwa tarehe 4/3/2022. |
| 9. | 29/2021 MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KINONDONI DAR ES SALAAM | Alex Mwasumbi dhidi ya KTC na wengine 4 | Kesi ya rufaa dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na Baraza la Ardhi na Nyumba Kibaha katika kesi No. 49/2010 | 14,000,000/= | Ipo katika hatua ya kutajwa tarehe 31/1/2022. |
| 10. | 449/2021<br><br>MAHAKAMA KUU DIVISHENI YA ARDHI DAR ES SALAAM | Alfred Boaz Koya dhidi ya KTC na Mwanasheria Mkuu wa Serikali | Mgogoro wa eneo lenye ukubwa wa ekari 11 lililopo Mwanalugali, Tumbi. Mdai akidai Halmashauri kuvamia eneo lake na kuligawa kwa watu wengine kinyume na taratibu na kuomba mahakama iingilie kati kwa kumuondoa mdaiwa katika eneo hilo na kurudishiwa eneo lake. | - | Shauri lipo katika hatua za kusikiliza mapingamizi yaliyowekwa na mdaiwa na imepangwa tarehe 20/1/2022. |
| 11. | 115/2019<br><br>BARAZA LA ARDHI NA | Telesphory Mtui dhidi ya Elifadhili Lema, KTC na | Mgogoro wa kiwanja Na. 192 'MD' Block 'E' Mwanalugali. | - | Shauri lipo katika hatua za kusikiliza maamuzi madogo |



Scanned with CamScanner

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | NYUMBA KIBAHA | Asha Salum Poto | Mdai anaomba mahakama iingilie kati kwa kumuondoa mdaiwa wa kwanza (Elifadhili Lema) katika eneo hilo na kurudishwa eneo lake. | | kutokana na mapingamizi ya awali yaliyowekwa na wadaiwa na imepangwa tarehe 10/2/2022. |
| 12. | 35/2014 BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KIBAHA | Ramadhani Mwinchande vs. KTC | Mgogoro wa ardhi Bokotimiza | 10,000,000/= | Ipo katika hatua ya kusikiliza maamuzi ya maombi ya kukazia hukumu yaliyoombwa na mdai Baraza la Ardhi na Nyumba Kibaha na imepangwa tarehe 22/3/2022. |

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe walipokea na kuipitisha taarifa ya Kitengo cha Sheria kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021.

**UKAGUZI WA NDANI**

**SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA KITENGO.**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kwa kipindi cha robo ya pili kimetekeleza shughuli zifuatazo ambazo zipo kwenye Mpango kazi wa Kitengo kwa mwaka 2021/2022.

i. Kufanya ukaguzi miradi ya maendeleo ya ujenzi wa machinjio, soko la kisasa, hospital ya wilaya, ujenzi wa nyumba ya mtumishi, ujenzi wa madarasa na zahanati pamoja na jengo la ofisi za Halmashauri.
ii. Kukagua Hesabu na Nyaraka za kifedha katika akaunti zote za Halmashauri ili kuona kama taratibu na Sheria za fedha zinafuatwa.
iii. Kuandaa taarifa ya Ukaguzi wa ndani robo ya kwanza, 2021 na kuwasilisha katika Mamlaka husika.
iv. Kukagua taratibu za manunuzi katika Kitengo cha Manunuzi kama Sheria na taratibu zinafuatwa.
v. Kuhudhuria na kuwasilisha taarifa ya Ukaguzi ya robo ya kwanza, 2021 kwenye kikao cha Kamati ya Ukaguzi.
vi. Kushiriki zoezi la uhakiki wa madeni ya serikali lililoendeshwa chini ya usimamizi wa ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa ndani wa serikali.

vii. Kushiriki mafunzo ya utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo yaliyotolewa na TASAF.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe walipokea na kuipitisha taarifa ya Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021.

**KITENGO CHA UCHAGUZI**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kitengo cha Uchaguzi kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba Disemba, 2021.

**KAZI ZILIZOTEKELEZWA**

**I. UPUNGUFU WA VIONGOZI WA SERIKALI ZA MITAA NA MADIWANI**

Katika kipindi cha robo ya pili kuanzia Oktoba hadi Desemba, 2021 Halmashauri ya Mji Kibaha imekuwa na nafasi wazi ya Diwani Kata ya Misugusugu baada aliyekuwa Mhe. Diwani wa Kata hiyo kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) **Mhe. John Simbawani Mwinami kufariki dunia tarehe 21/11/2021 na kuzikwa tarehe 25/11/2021.**

Aidha, taarifa ya kifo cha **Mhe. John Simbawani Mwinami** aliyekuwa Diwani wa Kata ya Misugusugu iliwasilishwa kwa **WAZIRI WA TAMISEMI** na Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kibaha kwa barua yenye Kumb. Na. KTC/E.50/137 ya tarehe 13/12/2021. Hivyo, Halmashauri ya Mji Kibaha ina nafasi wazi 01 ya Diwani Kata ya Misugusugu.

Uchaguzi Mdogo wa Diwani Kata ya Misugusugu utafanyika baada ya kupokea Taratibu, Mwongozo na maelekezo kutoka OR -TAMISEMI pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

**ii. KUANDAA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KITENGO CHA UCHAGUZI**

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Uchaguzi kimeshiriki katika maandalizi ya bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zote za Kitengo cha Uchaguzi kwa mwaka wa fedha ujao.

**iii. KUANDAA TAARIFA MBALIMBALI ZA KITENGO CHA UCHAGUZI**

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Uchaguzi kimeendelea kuandaa taarifa mbalimbali na kuziwasilisha mahali zinapohitajika kwa wakati.

**iv. CHANGAMOTO**

- Upungufu wa bajeti katika kutekeleza majukumu ya Kitengo cha Uchaguzi na hasa Uchaguzi Mdogo wa Viongozi wa Serikali Mitaa katika Mitaa miwili ambayo ina nafasi wazi za Wenyeviti wa Mitaa.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe walipokea na kuipitisha taarifa ya Kitengo cha Uchaguzi kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021.



18. Mansuetha Mb...



Scanned with CamScanner

**KITENGO CHA MAWASILIANO, HABARI, UHUSIANO NA TEHAMA**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha kuwa Kitengo cha Mawasiliano, Habari, Uhusiano na TEHAMA katika robo hii ya pili kimetekeleza shughuli zifuatazo;

**SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA KITENGO**

SEKTA YA TEHAMA

i. Kusimika miundombinu ya mfumo wa GoT-Homis (LAN) kwenye zahanati ya Kongowe na zahanati ya Misugusugu na kutoa elimu juu ya matumizi ya mfumo huo.
ii. Kufunga Mfumo wa GoTHomis (LAN) katika zahanati ya Misugusugu.
iii. Kuendelea kusimamia na kuhakikisha Mifumo iliyopo ambayo ni MUSE, HCMIS, LGRCIS, GoT-Homis, BEMIS, PREM, FFARS, TISS, MADENIMIS, CMG Planrep, selform, U5BRI n.k inafanya kazi kama inavyotakiwa.

SEKTA YA HABARI

i. Kuandaa habari 08 kwenye Magazeti na 05 Runinga na habari 11 redioni zinazoihusu Halmashauri.
ii. Kuandaa Vitambulisho 35 vya Watumishi wa ajira mpya, waliohamia na kupoteza.
iii. Kupiga picha 210 za Miradi ya Maendeleo hasa ujenzi wa miundombinu pamoja na Matukio Mbalimbali yanayoendelea Kwenye Halmashauri yetu ikiwemo ziara za Kimkoa na Kitaifa na Kuzitunza kama Kumbukumbu za Halmashauri.
iv. Kujibu Maswali 6 ya msingi na Maswali 6 ya ufafanuzi yanayohusu Halmashauri ya Kibaha toka Kwa Waandishi wa Habari.
v. Kuhuisha tovuti kwa kuweka miradi ya ujenzi wa madarasa ya UVIKO-19

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe waliipokea na kuipitisha taarifa ya Kitengo cha Mawasiliano, Habari, Uhusiano na TEHAMA kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2021.

**KFU/MUHT. NA. 13/02/2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

- Semina ya Morogoro na Kahama wajumbe walizitaka idara zinazohusika na utekelezaji wa mapendekezo ya ziara hizo waandae na kuwasilisha mpango kazi wa utekelezaji wa yale waliojifunza katika maeneo yao hasa suala la wajasiriamali.
- Mwenyekiti alikieleza kikao kuwa ataboresha kamati za kudumu za Halmashauri wa ajili ya ufanisi kadiri anavyoona inafaa hivyo, ni kuwa na kamati hai zinazoweza wasiidia kufanya wanatakiwa kazi.
- Mjumbe alieleza kuwa kutokana na upepo uliovuma nyakati za usiku umeezua paa ya madarasa mawili katika Shule ya Msingi Mwendapole aliomba Mwenyekiti na Mkurugenzi kufika eneo la tukio kuona hali ilivyo na kuona namna ya kufanya ukarabati.



Scanned with CamScanner

**KFU/MUHT. NA. 14/02/2022: KUFUNGA KIKAO:**

Mwenyekiti alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumaliza kikao salama pia aliwashukuru wajumbe kwa maoni yao kisha alifunga kikao saa 07:51 mchana.

**UMETHIBITISHWA NA:-**

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **MHE. MUSSA A. NDOMBA** | **ENG.MSHAMU A. MUNDE** |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |
| **TAREHE** 15-02-2022 | **TAREHE** 15-02-2022 |





Scanned with CamScanner